ISSN 0856 - 034X

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANI

*Supplement No. 23* *23rd JUNE, 2023*

*SUBSIDIARY LEGISLATION*

*To The Gazette of the United Republic of Tanzania No. 15 Vol. 104 Dated 23rd June, 2023*
Printed by The Government Printer, Dodoma by Order of Government

TANGAZO LA SERIKALI NA. 409 la tarehe 23/6/2023

SHERIA YA MADINI,
(SURA YA 123)

# KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 129)*

KANUNI ZA WAJIBU WA WAMILIKI WA LESENI ZA MADINI KWA JAMII ZA MWAKA 2023

## MPANGILIO WA KANUNI

*Kanuni* *Maelezo*

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

1. Jina.
2. Matumizi.
3. Tafsiri.

SEHEMU YA PILI
MPANGO WA WAJIBU WA MMILIKI WA LESENI YA MADINI KWA JAMII

4. Uandaaji wa mpango.
5. Kamati ya Wataalamu.
6. Muundo wa Kamati ya Wataalamu.
7. Majukumu ya Kamati.
8. Kuwasilisha mpango kwa halmashauri husika.
9. Kuwasilisha mpango kwa Mawaziri.



CamScanner

10. Vipaumbele vya jamii zilizopo katika eneo lenye shughuli za madini.

SEHEMU YA TATU
MASHARTI YA FEDHA

11. Fedha za mpango.
12. Hesabu na ukaguzi wa fedha.
13. Fedha za ziada.
14. Taarifa ya fedha na miradi.

SEHEMU YA NNE
UTEKELEZAJI WA MPANGO WA WAJIBU WA MMILIKI WA LESENI YA MADINI KWA JAMII

15. Utekelezaji wa mpango.
16. Usimamizi na ukaguzi wa utekelezaji wa mpango.
17. Utatuzi wa migogoro.

SEHEMU YA TANO
MASHARTI YA JUMLA

18. Elimu kuhusu wajibu wa mmiliki wa leseni.
19. Ukomo wa muda wa kutekeleza majukumu.
20. Miongozo au sheria ndogo za serikali za mitaa.
21. Makosa.



CamScanner

*Tangazo La Serikali Na. 409 (Linaendelea)*

SHERIA YA MADINI,
(SURA YA 123)

________

**KANUNI**

________

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 129)*

KANUNI ZA WAJIBU WA WAMILIKI WA LESENI ZA MADINI KWA JAMII ZA MWAKA 2023

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

Jina

1. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Wajibu wa Wamiliki wa Leseni za Madini kwa Jamii za mwaka 2023.

Matumizi

2. Kanuni hizi zitatumika kwa wamiliki wa leseni za madini zilizoainishwa katika Sehemu ya Nne ya Sheria.

Tafsiri

3. Katika Kanuni hizi, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"Kamati ya Wataalamu" maana yake ni Kamati ya Wataalamu kuhusu Wajibu wa Mmiliki wa Leseni ya Madini kwa Jamii itakayoanzishwa kwa mujibu wa kanuni ya 5;

"Mamlaka ya Serikali ya Mtaa" maana yake ni:

Sura ya 287

(a) halmashauri ya kijiji, halmashauri ya mji mdogo, kitongoji, halmashauri ya wilaya au mamlaka nyingine yoyote ya serikali za mitaa zilizoanzishwa chini ya Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya); au

Sura ya 288

(b) kata, mtaa, halmashauri ya mji, halmashauri ya manispaa au halmashauri ya jiji iliyoanzishwa chini ya Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji);

Sura ya 123

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Madini;



CamScanner

"Tume" maana yake ni Tume ya Madini ambayo imeanzishwa chini ya Sheria; na

"Waziri" maana yake ni Waziri mwenye dhamana ya masula ya madini.

## SEHEMU YA PILI
## MPANGO WA WAJIBU WA MMILIKI WA LESENI YA MADINI KWA JAMII

Uandaaji wa mpango

4.-(1) Mmiliki wa leseni ya madini atawajibika kuandaa mpango madhubuti wa wajibu wake kwa jamii kwa kushirikisha halmashauri ya kijiji au mtaa uliopo katika eneo lenye shughuli za madini kupitia halmashauri husika.

(2) Mmiliki wa leseni ya madini atakuwa na wajibu wa kushirikisha halmashauri ya kijiji au mtaa uliopo eneo lenye shughuli za madini katika kuainisha vipaumbele vya jamii zilizopo au zinazozunguka eneo hilo kwenye zoezi la uandaaji wa mpango wa wajibu wake kwa jamii.

(3) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (2), miradi itakayoibuliwa na halmashauri ya kijiji au mtaa itapaswa kujadiliwa na Kamati ya Maendeleo ya Kata kwa kumshirikisha mmliki wa leseni ya madini na kisha kuwasilishwa kwenye halmashauri ya wilaya, mji, manispaa au jiji husika kwa ajili ya uchambuzi na uhakiki ifikapo mwezi Oktoba kila mwaka.

(4) Kwa madhumuni ya kifungu cha 105(5) cha Sheria, jamii zilizopo au zinazozunguka eneo lenye shughuli za madini zitanufaika na mpango wa wajibu kwa jamii kwa utaratibu ufuatao:

(a) kiasi cha asilimia 40 kitatengwa kwa ajili ya miradi ya kijiji au mtaa ambapo shughuli za madini zinafanyika; na

(b) kiasi cha asilimia 60 kitatengwa kwa ajili ya miradi ya halmashauri ya wilaya, mji, manispaa au jiji husika ambako shughuli za madini zinafanyika.



CamScanner

Kamati ya Wataalamu

5. Kila halmashauri ya wilaya, mji, manispaa au jiji ambako shughuli za madini zinafanyika itaunda kamati ya wataalamu itakayoitwa Kamati ya Wataalamu kuhusu Wajibu wa Mmiliki wa Leseni ya Madini kwa Jamii.

Muundo wa Kamati ya Wataalamu

6. Kamati ya Wataalamu itaundwa na wajumbe wafuatao:

(a) Mkurugenzi Mtendaji ambaye atakuwa Mwenyekiti;
(b) Afisa Mipango ambaye atakuwa Katibu;
(c) Afisa wa Tume wa eneo husika;
(d) wawakilishi wawili wa mmiliki wa leseni ya madini;
(e) mhandisi;
(f) Wakili wa Serikali;
(g) Afisa Mazingira;
(h) Afisa Maendeleo; na
(i) afisa kutoka katika mradi mahsusi unaotekelezwa na mpango husika.

Majukumu ya Kamati

7.-(1) Kamati itakuwa na majukumu yafuatayo:

(a) kupitia mipango, michoro, ratiba ya utekelezaji na masuala mengine yanayohusiana na wajibu wa mmiliki wa leseni kwa jamii na kuwasilisha kwa halmashauri ya wilaya, mji, manispaa au jiji;
(b) kuhakikisha kuwa miradi inayotekelezwa na wamiliki wa leseni inazingatia thamani ya fedha;
(c) kusimamia ubora wa vifaa na miundombinu pamoja na ufanisi katika utekelezaji wa miradi;
(d) kufuatilia na kuhakikisha miradi iliyoidhinishwa chini ya mipango inatekelezwa kwa wakati;
(e) kufuatilia uzingatiaji na ufanisi katika utekelezaji wa sera ya mmiliki wa leseni kuhusu wajibu wake kwa jamii;
(f) kutoa ushauri wa kitaalamu kwa watekelezaji wa miradi; na
(g) kuandaa taarifa ya utekelezaji wa miradi na



CamScanner

kuiwasilisha kwa halmashauri ya wilaya, mji, manispaa au jiji.

(2) Kamati ya Wataalamu ya halmashauri ya wilaya, mji, manispaa au jiji husika itachambua na kuhakiki mpango uliowasilishwa chini ya kanuni ndogo ya (1) ndani ya muda wa siku kumi na nne tangu ulipopokelewa na kuuwasilisha katika halmashauri ya wilaya, mji, manispaa au jiji husika ukiwa pamoja na ushauri wa Kamati hiyo.

Kuwasilisha mpango kwa halmashauri husika

8.-(1) Kila halmashauri ya wilaya, mji, manispaa au jiji itapitia na kupitisha mpango uliowasilishwa ndani ya siku saba tangu ulipowasilishwa na Kamati ya Wataalamu, na iwapo haitaridhika na maudhui ya mpango huo, inaweza, kwa kuzingatia kanuni ya 10, kuukataa na kuelekeza mpango huo urejeshwe kwa mmiliki wa leseni ya madini kwa ajili ya maboresho.

(2) Endapo halmashauri ya wilaya, mji, manispaa au jiji itaukataa mpango na kuurejesha kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (1) itapaswa kuwasilisha kwa mmiliki wa leseni sababu za kuukataa mpango huo.

(3) Mmiliki wa leseni ya madini atawajibika kuboresha mpango kulingana na maelekezo ya halmashauri ya wilaya, mji, manispaa au jiji na kwa mujibu wa masharti ya Sheria na kuwasilisha tena kwenye halmashauri ya wilaya, mji, manispaa au jiji husika.

(4) Endapo kutakuwa na mkwamo wowote katika kuafikiana kati ya halmashauri ya wilaya, mji, manispaa au jiji husika na mmiliki wa leseni ya madini kuhusu uandaaji na upitishaji wa mpango, mkwamo huo utatatuliwa na Mkuu wa Mkoa katika halmashauri husika.

Kuwasilisha mpango kwa Mawaziri

9.-(1) Endapo halmashauri husika itaridhika na maudhui ya mpango wa wajibu kwa jamii uliowasilishwa na mmiliki wa leseni ya madini, halmashauri hiyo itauwasilisha mpango huo kwa Waziri mwenye dhamana na masuala ya serikali za mitaa na Waziri mwenye dhamana ya masuala ya fedha ndani ya siku thelathini tangu kupokelewa kutoka kwa mmiliki wa leseni ya madini.



CamScanner

(2) Waziri mwenye dhamana ya masuala ya serikali za mitaa kwa kushirikiana na Waziri mwenye dhamana ya masuala ya fedha wataunda Kamati ya Pamoja ambayo jukumu lake litakuwa ni kuwashauri Mawaziri husika kuhusu mipango ya wajibu wa wamiliki wa leseni kwa jamii inayowasilishwa kwa ajili ya idhini.

(3) Kamati ya Pamoja itaandaa taarifa na kuiwasilisha kwa Mawaziri, na iwapo Mawaziri-

(a) wataridhika na maudhui ya mpango huo kulingana na Sera za Serikali za Mitaa na Sera za Fedha watawasilisha mpango huo kwenye halmashauri ndani ya kipindi cha siku kumi na nne tangu tarehe ya kuupokea mpango huo kutoka kwenye halmashauri; au

(b) hawataridhika na maudhui ya mpango huo kulingana na Sera za Serikali za Mitaa na Sera za Fedha, wataurejesha mpango huo kwenye halmashauri ndani ya kipindi cha siku kumi na nne tangu tarehe ya kuupokea mpango huo ukiwa na maelekezo mahususi.

(4) Bila kuathiri utaratibu ulioainishwa chini ya kanuni ndogo ya (1), (2) na (3) endapo utapita muda wa siku ishirini na moja bila halmashauri husika kupokea majibu tangu tarehe ambayo Mawaziri walipokea mpango huo, itahesabika kuwa mpango umeridhiwa na halmashauri itamjulisha mmiliki wa leseni kuendelea na utekelezaji kwa kuzingatia muda uliokubaliwa kwenye mpango.

(5) Halmashauri ya wilaya, mji, manispaa au jiji itawasilisha mpango ulioridhiwa kwa mmiliki wa leseni ndani ya siku saba baada ya kuupokea kutoka kwa Mawaziri na mmiliki huyo atauwasilisha mpango huo kwenye Tume ndani ya siku saba tangu alipoupokea kutoka halmashauri husika.

Vipaumbele vya jamii zilizopo katika eneo lenye

10. Mmiliki wa leseni ya madini na halmashauri husika watahakikisha kuwa miradi yote itakayotekelezwa chini ya mpango uliokubaliwa kwa pamoja-

(a) inazingatia masuala ya kimazingira, kijamii,

shughuli za madini

kiuchumi na kitamaduni kulingana na vipaumbele vya jamii husika;

(b) inaweza kupimika kwa vigezo vya manufaa na mafanikio;

(c) inatekelezeka; na

(d) inakamilika ndani ya muda ulioafikiwa.

## SEHEMU YA TATU
## MASHARTI YA FEDHA

Fedha za mpango

11. Mmiliki wa leseni ya madini atawajibika-

(a) kutenga fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mpango wa wajibu kwa jamii zilizopo eneo lenye shughuli za madini kwa kila mwaka;

(b) kugharamia miradi yote iliyo chini ya mpango wa wajibu kwa jamii kulingana na mpango uliokubaliwa; na

(c) kutoa taarifa ya maandishi kwa halmashauri husika na Tume kuhusu malipo yote yaliyofanywa kwa wakandarasi, wakandarasi wadogo au washirika wengine waliotekeleza miradi.

Hesabu na ukaguzi wa fedha

12.-(1) Fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi chini ya mpango wa wajibu kwa jamii zitakaguliwa na Tume kulingana na viwango vya ukaguzi.

(2) Endapo fedha zilizotengwa hazitatumika kwa namna yoyote ile, mmiliki wa leseni ya madini atakuwa na wajibu wa kutoa taarifa na sababu kwa halmashauri husika na Tume kuhusu fedha zilizotengwa kutokutumika kwa ajili ya utekelezaji wa mradi au miradi katika mwaka wa fedha husika.

(3) Fedha zilizotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi au miradi iliyoafikiwa na mmiliki wa leseni na halmashauri ya wilaya, mji, manispaa au jiji kwa kila mwaka wa fedha, zitatolewa na kutumika ndani ya mwaka wa fedha husika, na endapo fedha iliyotengwa haikutumika



CamScanner

katika mwaka wa fedha husika, fedha hiyo itatumika katika mwaka wa fedha unaofuata na haitaathiri miradi mingine iliyopangwa kutekelezwa katika mpango wa mwaka huo.

Fedha za ziada

13.-(1) Iwapo kutakuwa na kiasi cha fedha kitakachobaki baada ya kutekeleza mradi husika, kiasi hicho cha fedha kitatumika kugharamia miradi mingine inayokusudiwa kutekelezwa baada ya pande zote kufikia muafaka.

(2) Endapo kutakuwa na kazi ambazo hazijakamilika katika utekelezaji wa mradi uliopo kwenye mpango kutokana na kiwango cha fedha kilichotengwa kutokutosheleza, mmiliki wa leseni atazingatia kiwango hicho cha fedha katika mpango wa mwaka unaofuata.

Taarifa ya fedha na miradi

14. Mmiliki wa leseni ya madini atawajibika kuwasilisha kwa Tume taarifa kuhusu fedha zilizotumika na miradi iliyotekelezwa ndani ya siku kumi na nne kila baada ya robo ya mwaka wa kalenda na taarifa ya mwaka ndani ya siku sitini baada ya tarehe 31 Desemba.

## SEHEMU YA NNE
## UTEKELEZAJI WA MPANGO WA WAJIBU WA MMILIKI WA LESENI YA MADINI KWA JAMII

Utekelezaji wa mpango

15.-(1) Mmiliki wa leseni ya madini atawajibika kutekeleza mpango wa wajibu wake kwa jamii kwa kuzingatia taratibu za ununuzi na anaweza kumwajiri mkandarasi au mtu mwingine yeyote katika utekelezaji wa miradi iliyopo kwenye mpango.

(2) Katika utekelezaji wa mpango mmiliki wa leseni ya madini atawasilisha taarifa ya utekelezaji wa mpango ya kila robo mwaka kwenye halmashauri husika na Tume.

Usimamizi na ukaguzi wa utekelezaji wa mpango

16.-(1) Halmashauri itawajibika kusimamia utekelezaji wa mpango na itakuwa na haki zifuatazo:

(a) kukagua mikataba yoyote, makadirio ya kiasi (BOQ) au nyaraka nyingine zinazohusiana na

utekelezaji wa mpango; na

(b) kupewa taarifa za msingi zinazohusiana na mpango kutoka kwa mmiliki wa leseni ya madini au mtu au kampuni inayohusika na utekelezaji wa mpango.

(2) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1), miradi inayotekelezwa chini ya mpango wa wajibu kwa jamii itakaguliwa na halmashauri husika kila robo mwaka wa fedha na taarifa ya ukaguzi itawasilishwa kwa Tume.

(3) Tume itawajibika kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa mpango wa wajibu wa mmiliki wa leseni ya madini kwa jamii kwa mujibu wa Sheria.

(4) Katika kutekeleza kanuni ndogo ya (1) na (2), ukaguzi kuhusiana na utekelezaji wa mpango utafanywa kwa kuzingatia thamani halisi ya fedha na kazi iliyofanyika, na katika kuthibitisha na kupima kama mradi husika umejengwa kwa thamani fulani, vigezo vya bei na ubora vitatumika.

(5) Mmiliki wa leseni ya madini na halmashauri husika wanapaswa kutunza taarifa za fedha zilizotolewa katika mpango wa wajibu wa wamiliki wa leseni kwa jamii na kwenye miradi inayoendelea kutekelezwa na iliyotekelezwa kwa kipindi cha angalau miaka mitano.

Utatuzi wa migogoro

17.-(1) Bila kuathiri masharti ya Sheria na Kanuni hizi, endapo kutakuwa na mgogoro kati ya mmiliki wa leseni ya madini na halmashauri husika katika utekelezaji wa mpango, mgogoro huo utatatuliwa kwa njia ya mazungumzo ya amani.

(2) Endapo pande zote zitashindwa kutatua mgogoro huo kwa njia ya mazungumzo ya amani, upande usioridhika utawasilisha mgogoro huo kwa Tume ndani ya siku saba tangu waliposhindwa kuafikiana, na Tume itatoa uamuzi ndani ya siku kumi na nne.

(3) Endapo kuna upande ambao hautaridhika na uamuzi wa Tume, upande huo utakuwa na haki ya kukata rufaa kwa Waziri ndani ya siku saba tangu tarehe ya uamuzi wa Tume, na Waziri atatoa uamuzi wake ndani ya siku



CamScanner

*Tangazo La Serikali Na. 409 (Linaendelea)*

thelathini.

## SEHEMU YA TANO
## MASHARTI YA JUMLA

Elimu kuhusu wajibu wa mmiliki wa leseni

18. Kila halmashauri na mmiliki wa leseni ya madini kwa kushirikiana na Wizara yenye dhamana ya masuala ya madini watatoa elimu kwa umma angalau mara mbili kwa mwaka kuhusu wajibu wa wamiliki wa leseni za madini kwa jamii.

Ukomo wa muda wa kutekeleza majukumu

19.-(1) Endapo yeyote kati ya mmiliki wa leseni au halmashauri atashindwa kutekeleza majukumu ndani ya muda ulioainishwa chini ya Kanuni hizi, anaweza kuomba nyongeza ya muda kwa Waziri na kubainisha sababu za msingi za maombi ya nyongeza hiyo.

(2) Waziri anaweza kuongeza muda ambao hautazidi siku thelathini au kukataa ombi hilo na atatoa sababu.

(3) Endapo Waziri atakubali maombi ya kuongeza muda, mmiliki wa leseni au halmashauri atatakiwa kutekeleza jukumu hilo ndani ya muda utakaobainishwa na Waziri bila nyongeza nyingine.

Miongozo au sheria ndogo za serikali za mitaa

20. Miongozo au sheria ndogo zitakazoandaliwa na serikali za mitaa kwa mujibu wa kifungu cha 105 cha Sheria zitapaswa kuzingatia masharti ya Kanuni hizi.

Makosa

21. Mmiliki wa leseni ya madini atakayeshindwa kutekeleza masharti yaliyoainishwa chini ya Kanuni hizi atakuwa ametenda kosa chini ya Sheria na atachukuliwa hatua kwa mujibu wa kifungu cha 63 cha Sheria.

Dodoma,
15th June, 2023

DOTO MASHAKA BITEKO
*Waziri wa Madini*



CamScanner